

SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA PANGANI  
IDARA YA KISWAHILI  
MTIHANI WA KUTANGULIA WA MWIGO  
KIDATO CHA 4

102/3

KARATASI YA 3

FASIHI

MACHI, 2013

MUDA: SAA 2 ½

**Maagizo.**

- Jibu maswali manne pekee.
- Swali la kwanza ni la lazima.
- Maswali mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu tatu zilizobaki; yaani Hadithi fupi, Ushairi na Fasihi simulizi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

For More Free KCSE Past Papers Visit [www.freekcepastpapers.com](http://www.freekcepastpapers.com)

## **SEHEMU YA A : UTENGANO**

### **Swali la lazima.**

1. a) Eleza aina tano za migogoro inayojitokeza katika riwaya ya Utengano. (al 10)
- b) Onyesha jinsi mbinu ya hadithi ndani ya hadithi ilivyotumika katika riwaya ya Utengano. Rejelea hadithi zozote tano. (al 10)

## **SEHEMU YA B: HADITHI FUPI**

### **KEN WALIBORA NA SAID A MOHAMED: DAMU NYEUSI**

Jibu swali la 2 au la 3.

2. “Msifikiri kwamba Mzungu anatupenda sisi watu weusi.”
  - a) Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi husika. (al 14)
  - b) Fafanua sifa 3 za mhusika anayeyanukuu maneno haya. (al 6)
3. “Mwakumbuka katika safari ya kwenda angani namna ndege walivyoshirikiana naye...”
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
  - b) Ni mbinu gani mbili zilizotumiwa katika dondoo hili? (al 2)
  - c) Kisa katika dondoo hili kina mshabaha na hadithi nzima. Eleza kwa fasili mshabaha huu. (al 14)

## **SEHEMU YA C: USHAIRI**

Jibu swali la 4 au 5.

### **4. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye *zani*, kweli mja hapendekei,  
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki,  
Ukweliwe haafiki, njama zake zi Moyoni, usimwone ni rafiki,  
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,  
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakizifuata nyago,  
Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,  
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Pindi kinunua kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo,  
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo,  
Tamko lake “Subutu!” kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,  
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,  
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,  
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,  
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo,  
Bahati ina hadaa, kukupa alo sodawi, aibatili rohoyo,  
*Mipangoyo kwake jaa*, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaniyo,  
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,  
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa mazito kuambiwa,  
Ama nitimue mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,  
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

### **Maswali.**

- a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (al 1)
- b) Mtungaji / mshairi analalamika juu ya nini? (al 3)
- c) Hili ni shairi la bahari gani? Toa sababu. (al 2)
- d) Kifafanue kibwagizo cha shairi hili. (al 2)
- e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (al 4)
- f) Kwa kurejelea mifano kutoka katika shairi taja na ufafanue mbinu mbili za lugha alizotumia mshairi. (al 4)
- g) Kwa kurejelea ubeti wa sita thibitisha matumizi ya unuru wa mshairi. (al 2)
- h) Eleza maana ya maneno haya jinsi yalivyotumika katika shairi. (al 2)
- (i) zani
- (ii) mipangoyo kwake jaa.

### **5. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

#### **Uneni Wao**

Zamani  
Zamani sana  
Nilimwona mama na kitoto kifuani  
Niliona lesa likitamba ardhini la bi kizee  
Niliona kaputi la mzee mkuu mchangani  
Niliona vivulana na visichana  
Niliona niliona, Niliona!

Zamani  
Zamani sana  
Zama kabla nijue kuvaa kaptura  
Nikasikia wakiamba yangu  
"Kiongozi wa Kesho" wakakariri  
Pindi ukifika wao mwisho  
Nitavalishwa mavisho  
Zamani  
Zamani sana  
Siku za kupigana na simi  
Nilisikia na masikio yangu

Sauti ikienda mbinguni  
“Hii ni mikakati ya wetu wajukuu”  
Ndoto zangu zikawa kule.  
Na leo?  
Si zamani sana  
Amekalia mwengine na mwengine  
Ingawa naona wimbo ungalipo!  
Ningali mtoto ijapo kichwa ni cheupe pe?  
Nangoja kesho!

### **Maswali.**

- a) Fafanua anwani ya shairi hili. (al 1)
- b) Eleza ujumbe wa shairi hili. (al 5)
- c) Eleza dhana ya mishata kama ilivyojitokeza katika shairi hili. (al 4)
- d) Eleza sababu ya mshairi kutumia alama ya kiulizi katika mshororo huu  
.....”Na leo?” (al 2)
- e) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha kwa kutoa hoja tatu. (al 4)
- f) Fafanua toni ya shairi hili. (al 3)
- g) Taja mbinu iliyotumiwa katika mshororo ufuatao: “Nitavalishwa mavisho” (al 1)

### **SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI**

- a) Eleza maana za dhana zifuatazo katika Fasihi Simulizi.
- (i) Maapizo (al 2)
- (ii) Mawaidha (al 2)
- b) Huku ukirejelea hoja mbilimbili jadili umuhimu na udhaifu wa mbinu ya kushiriki katika utafiti wa fasihi simulizi. (al 8)
- c) Eleza jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuhifadhi au kuendeleza fasihi simulizi. (al 4)
- d) Michezo ya watoto ina hasara gani? Jadili hoja zozote mbili. (al 4)